# TAARIFA KWA UMMA JUU YA USALAMA WA MBOGAMBOGA

**Dar es Salaam, 29 Septemba 2025**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) pamoja na majukumu mengine hufanya ufuatiliaji wa bidhaa za mbogamboga ili kuhakiki usalama wake. Kilimo cha mazao ya mbogamboga, hutumia viuatilifu ili kukabiliana na wadudu waharibifu, magonjwa ya mimea na magugu ambapo viuatilifu vinavyotakiwa kutumika ni vile vilivyoidhinishwa na mamlaka za udhibiti.

Ufuatiliaji na uchunguzi wa kimaabara wa aina mbalimbali za mbogamboga katika soko umeonesha kuwa mazao hayo hayana mabaki ya viuatilifu (pesticide residues) yanayozidi kiasi kinachovumilika (maximum residue limit) kwa mujibu wa viwango vya WHO/FAO.

TBS itaendelea kufanya ufuatiliaji wa bidhaa za mbogamboga na kushirikiana na Mamlaka inayohusika na udhibiti wa afya ya mimea na viuatilifu ili kuhakikisha usalama wa mbogamboga unazingatiwa na wadau wote katika mnyororo wa thamani.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba **0800110827.**

Imetolewa na:

Gladness H. Kaseka
**Maneja wa Uhusiano na Masoko**

*"Kuchochea Ubora na Usalama kwa Maisha Bora"*